# Kushirikisha Kikamilifu Kupitia Shule ya Sabato

MPANGOKAZI WA
KUIHUISHA UPYA
SHULE YA SABATO

2017 – 2020

Shule ya Sabato GC na
Idara ya Huduma Binafsi



Adopted From GC
By Pr. Almodad Amos

# KUUFIKIA ULIMWENGU

## Kuihuisha Shule ya Sabato kwa

### kuhimiza makusudi ya msingi ya Shule ya Sabato

"Bwana anatamani wale ambao wanahusika katika Shule ya Sabato wawe Wamishenari, wenye uwezo wa kuiendea miji na vijiji vinavyolizunguka kanisa, na kuwapatia nuru ya uzima wale wanaokaa katika giza."

---- *Testimonies for Sabbath School, Uk. 74*





# KUSHIRIKISHWA KIKAMILIFU KATIKA SHULE YA SABATO

"Kusudi la Shule ya Sabato linapaswa kuwa ukusanyaji wa roho."

*—Counsels on Sabbath School Work, uK. 61.*

## Utume Wetu

Utume wa Idara ya Shule ya Sabato ni kutengeneza mfumo wa Elimu ya Kiroho unaoijenga Imani ya Waadventista Wasabato na Mwenendo wao. Shule ya Sabato Inajenga imani kwa kuwahimiza watu kujifunza Biblia na Maandiko ya Roho ya Unabii. Inajenga tabia kwa kutumia maishani kanuni za maisha za Kibiblia; na kwa kumtia moyo kila mshiriki wa Shule ya Sabato kuishi kulingana na mafundisho ya Kanisa la Waadventista Wasabato

**Goli Letu:** *Kufanya Wanafunzi!*

MPANGOKAZI WA KUIHUISHA UPYA SHULE YA SABATO


2017 – 2020

Shule ya Sabato na Huduma Binafsi

## A. KUMFIKIA MUNGU [Kwa Kujifunza Biblia & Kwa Maombi ]

Kila siku mshiriki ajifunze Biblia na kufanya maombi *akitumia miongozo ya kujifunza Biblia*


1. **KWA NINI KUMFIKIA MUNGU?** Kwa sababu suala la kuielewa Biblia ni muhimu sana kwa maisha yetu ya kiroho na kwa kuutambua utume wetu.



**GOLI LETU:** Kuwashirikisha washiriki wa Shule ya Sabato katika program ya Kujifunza Biblia na kuwa na Ibada makini ya maombi kila siku.

**KIPIMO:** *(Viashiria vya Mafanikio)*

- ▶ Kuona washiriki wote wamewekwa katika vikosi vya utendaji vya Shule ya Sabato na kupima uhai wa utendaji wa kila kikosi ktk kutimiza makusudi ya Shule ya Sabato. Tumia Taarifa za kila juma, za shule ya Sabato, ili kupima mafanikio ya kikosi.
- ▶ Kuona viongozi wa Shule ya Sabato wakipata semina (Hasa waalimu) juu ya namna ya kuwaongoza wanakikosi wake kuisoma Biblia na namna ya kufanya Ibada wakiwa nyumbani.
- ▶ Kuongezeka kwa idadi ya washiriki wanaojifunza Biblia kwa kutumia miongozo ya kujifunza Biblia, kila siku.
- ▶ Kuongezeka kwa Idadi ya watu wanaohudhuria Shule ya Sabato.
- ▶ Kuongezeka kwa Idadi ya Waaminifu katika matoleo na katika mahudhurio ya Ibada kanisani.
- ▶ Kuona washiriki wa Shule ya Sabato wakifanyika wanafunzi na wakifanya wanafunzi.
- ▶ Kuona waalimu wa shule ya Sabato Wakifundisha Miongozo ya Kujifunza Biblia kwa namna ambayo kila mwanakikosi anashiriki ktk mjadala. *(Hii itakuwa udhirisho kuwa watu wamekutana na Mungu tangu nyumbani).*




Muundo wa Kumshirikisha Kila mshiriki wenye sehemu 3: KUMFIKIA MUNGU, KUWAFIKIA WENZETU na KUUFIKIA ULIMWENGU, unajengwa juu ya agizo la KUFANYA WANAFUNZI na ndio unaitwa KUUFIKIA ULIMWENGU.

## 2. KWA NINI PROGRAM YA KUMFIKIA MUNGU?:

Hii ni kwa sababu ukweli wa Biblia unapaswa kujulikana kwa kila mtu. Lakini pia utafiti unatueleza wazi kuwa wengi wetu hawajakomazwa katika ufahamu wa mafundisho ya kweli za Biblia.



**GOLI LETU:** Kuwaongoza washiriki wote wa shule ya Sabato wa Kila Rika, kujifunza Biblia kwa kupitia mwongozo wa kujifunza Biblia uliotengenezwa ili kuwasaidia washiriki kuielewa Biblia na kile Mungu anachotufundisha kwa kupitia Biblia takatifu.

**KIPIMO:** *(Viashiria vya Mafanikio)*

- Kuona viongozi wa Vikosi vya Shule ya Sabato wakisimamia vizuri zoezi la kuwaongoza wanakikosi kutimiza kusudi la kujifunza miongozo hii wakiwa nyumbani ili kuyaelewa mafundisho ya Biblia. Pia kila kiongozi ahakikishe kila mtu anao Mwongozo wake Binafsi wa kujifunzia Biblia.
- Kadri siku zinavyokwenda, wanakikosi watakuwa wakikua katika kuielewa Biblia na itadhihirika wazi kwao kuwa Imani zote za Msingi za Waadventista Wasabato zinatokana na msingi wa Neno la Mungu. Kiongozi atafute muda wa kujadiliana na kikosi kuhusu umuhimu wa kujifunza Biblia.
- Kiongozi wa Shule ya Sabato amuone kiongozi wa Huduma Binafsi, Mzee wa Kanisa na wamuombe Mchungaji ili waweke mpango unaotekelezeka kwa haraka wa jinsi ya kuwafundisha wanakikosi juu ya: fundisho kuhusu Karama ya Roho ya Unabii, Historia ya Waadventista na mafundisho yanayozungumzia mambo yajayo (Unabii). Kisha wapange namna ya kuwapatia miongozo ili wanakikosi wajisomee wakiwa nyumbani.
- Katika mpango huu wa kumfikia Mungu, kiongozi wa Shule ya Sabato upande wa watoto (Kiongozi wa Huduma za Watoto) ashirikiane na viongozi wa Shule ya Sabato katika kuwaingiza watoto kwenye program hii ya Kumfikia Mungu (Yaani kuwakuza kiroho watoto) kwa kadri miongozo ya huduma za watoto zinavyoelekeza.

## B. KUWAFIKIA WENZETU [ Kutimiza Kusudi la Ushirika ktk Shule ya Sabato]

Mpango wa kutilia mkazo huduma ya ushirika katika kutimiza utume wa Kanisa.

**KWA NINI KUWAFIKIA WENZETU?** Ni kwa sababu Kanisa limeitwa kuwa jamii ya kiroho iliyojaa upendo, kila mtu kumjali mwenzake, kwa kuaksi upendo wa Mungu na uwepo wake.



**GOLI LETU:** Kuimarisha umoja wa jamii ya washiriki wote wa wa Shule ya Sabato.

**KIPIMO:** *(Viashiria vya Mafanikio)*

- Kila kikosi cha Shule ya Sabato kuweka ratiba ya kumtembelea angalau mwanakikosi mmoja kwa juma. Lakini pia kuwatembelea wagonjwa, waliorudi nyuma na watu ambao wanamatatizo flani yanayowasibu.
- Pia viongozi wa shule ya sabato washirikiane na kiongozi wa Huduma za Familia kuzihimiza familia kutembeleana. Kila Familia iwe na familia rafiki na waweke ratiba ya kutembeleana angalau mara moja kwa mwezi kadri nafasi inavyoruhusu.
- Kiongozi wa Huduma, Shule ya Sabato wamuombe Mzee wa Kanisa anayeshughulika na Kamati ya Malezi na Urejeshwaji kushirikiana nao katika kuwafundisha washiriki wa shule ya Sabato jinsi ya kushiriki katika program ya malezi na urejeshwaji. na utekelezaji uanze mara moja.
- Wazee wa Kanisa na Mchungaji, watafute muda wa ***kuwafundisha washiriki jinsi ya kutatua migogoro inayoweza kujitokeza ktk Kanisa***. Ni wajibu wa kiongozi kuwakumbusha mpaka litakapotekelezwa.
- Kuwatia moyo washiriki wa Shule ya Sabato kukutana kwa nia ya kujenga urafiki wa kawaida.
- Kiashiria muhimu kabisa ni kuona Idara husika katika kila kipengele ikishirikiana na Idara zingine katika kukamilisha utume; mkakati huu unahitaji kila idara ihusike kwa namna flani.

## C. KUWAFIKIA WENGINE: [ Kutimiza Kusudi la Kiutume ktk Shule ya Sabato]

Kuwahimiza Washiriki kushiriki ktk utume kwa jamii inayotuzunguka na ulimwenguni kote

**KWA NINI KUWAFIKIA WENGINE?** Kwa sababu huu ndio utume wetu. Makusudi ya kuwepo kwa kanisa ni pamoja na kuwaeleza wengine habari za upendo wa Mungu na jinsi anavyotamani kila mtu aokolewe.

Kazi yetu kubwa baada ya kuipokea ile nuru, ni kumtangaza Yesu kila fursa inapopatikana ili Dunia Yote imjue Mungu wetu na ili kila anayeamini aupokee wokovu.

**GOLI LETU:** Kuwatia moyo viongozi, waalimu na viokosi vya Shule ya Sabato kuhusika na kutekeleza mkakati wa Huduma Binafsi katika kuuwasilisha Ujumbe wa Malaika Watatu kwa jamii inayotuzunguka. Kazi ya viongozi ni kuwasaidia washiriki kuelewa jinsi jambo hili linavyofanyika kupitia semina.

**KIPIMO:** *(Viashiria vya Mafanikio)*



- Kwanza liongoze Kanisa kuiombea jamii inayowazunguka. Kisha kiongozi wa Shule ya Sabato ashirikiane na kiongozi wa Huduma binafsi ktk kutekeleza mpango wa Makanisa Yanayokua kwa kuanza na mikakati ya matendo ya Huruma kwa jamii.
- Anzisha makanisa kwa kutumia 'Matawi ya Shule ya Sabato.'
- Weka program ya kuliombea Kanisa Mahalia na Kanisa la Ulimwengu na utume wake.
- Angalau mara mbili kwa mwezi kamati ya Shule ya Sabato ikae kutathmini ongezeko la ushiriki wa wanakikosi katik utume kwa kupitia taarifa za Shule ya Sabato.
- Siri ya mafanikio katika kuihuisha upya Shule ya Sabato ni kuhakikisha kila mshiriki wa shule ya sabato anashiriki kikamilifu katika utekelezaji wa kile anachojifunza ktk shule ya Sabato na anaposhiriki katika utume wa Kanisa kupitia kikosi chake.
- Kiongoze kila kikosi kuwa na program flani ya kuihudumia jamii inayowazunguka kwa kuonesha matendo ya huruma.
- Watambue watu wote waliomo Kanisani na uhakikishe kila mmoja anashiriki kikamilifu ktk program zote za Shule ya Sabato. Asiwepo mtu atakayekuwa kama mtazamaji Kanisani.
- Kiongozi aliombe Kanisa kutenga muda wa kulielimisha Kanisa juu ya umuhimu wa matoleo ya Sadaka katika utimizwaji wa utume wa Kanisa.

## Hatimaye Tunatarajia yafuatayo:

### Kumsaidia Kila Mshiriki:

- Kuwa mwanafunzi wa Yesu kwa vitendo na sio ktk nadharia.
- Kukua katika ufahamu wa neno la Mungu kwa kupitia ufundishaji mzuri wa miongozo ya Biblia na mijadala ya vikundi vidogo vidogo.
- Kuelewa Historia, Theolojia na Msingi wa kibiblia wa Utume wa Kanisa la Waadventita Wasabato.
- Kuimarisha mahusiano ya vikosi vya Shule ya Sabato na ushiriki wao ktk utume.
- Kuwa na mwamko wa urejeshaji wa washiriki waliorudi nyuma na waliopoa.
- Kujua jinsi ya kukiongoza kikosi cha shule ya sabato ili kufanya huduma kwa jamii.
- Kuwafundisha washiriki wa shule ya sabato kuwa wainjilisti.
- ufundishaji wa namna ya uongozi bora wa kikosi cha shule ya sabato.

## JINSI YA KUMSHIRIKISHA KILA MSHIRIKI KTK SHULE YA SABATO

*Tenga dakika 15* kila kikosi kinapokutana kwa mipango, maombi na ushirika.*

- **KUWAFIKIA WENZETU:** Darasa lipange kutembeleana, kuomba pamoja, kuwatembelea waliorudi nyuma na kumpatia kila mtu sehemu ya kufanya katika hayo. Darasa limuombe Mungu kuwafunulia namna ya kuhudumia kwa familia zisizojiweza, vijana, waliorudi nyuma, wanawake na wanaume, na pia waziombee familia zote kujihusisha na huduma za kiutume.
- **KUWAFIKIA WENGINE:** Kila kanisa liombee na kujadili njia za kuifikia jamii inayowazunguka, mji/jiji na ulimwengu kwa kusudi la kutimiza agizo kuu la kuihubiri Injili kwa kupanda, kuvuna na kutunza wanaopatikana. Mchungaji ahakikishe kila idara inahusishwa katika kuweka malengo haya ya huu mpangokazi. Mchungaji ahakikishe magoli ya muda mfupi na magoli ya muda mrefu yote yanawekwa na hatua za utekelezaji zinaanza mara moja. TMI inamtaka kila mmoja kushiriki katika kuifikia jamii, hapa kuna mambo machache juu ya namna ya kujihusisha na TMI: **1. Kuwa na tabia ya kuchunguza mahitaji ya jamii inayokuzunguka. 2. Weka mkakati wa kuyashughulikia hayo mahitaji. 3. Omba Roho wa Mungu akuwezeshe kuyafikia malengo ya mkakati uliouweka.**
- **KUWAFIKIA WENGINE:** Wahimize washiriki kufanya Ibada za Nyumbani na kufanya Ibada Binafsi.

| TMI | Muda | Maelezo |
|---|---|---|
| Huduma za Ushirika<br>Huduma za Kiutume | Dakika 15.* | Omba, Panga, Gawa majukumu, Wafikirie waliorudi nyuma, Weka ratiba, Kisa cha utume, Himiza Utoaji. |
| Kujifunza Biblia | Dakika 45.* | Muhusishe kila mtu katika kuijadili somo la juma hilo. Uliza maswali na fafanua kwa jinsi ya muhtasari. |
| Chakula Cha Mchana | | Wakati mwingine kikosi kipange kula pamoja mlo wa mchana. **KISHA MTOKE WOTE KUMWENDEA MTU FLANI!** |

*Kila Kikosi Kiwe na Ratiba ya Siku ya Sabato. Kwa mfano huu hapo juu.

Sabbath School and Personal Ministries

General Conference Sabbath School and Personal Ministries Department
12501 Old Columbia Pike | Silver Spring, MD 20904 | 301-680-6182